

Yezebeli, alikuwa ni Binti wa Mfalme wa Wasidoni aliyeitwa Ethbaali (**1 Wafalme 16:31**). Sidoni ilikuwa ni nchi iliyokuwepo Kaskazini mwa Taifa la Israeli, kwasasa nchi hiyo ni nchi ya **LEBANONI**.

Desturi za Wasidoni zilikuwa ni kuabudu miungu, waliabudu mungu wao maarufu aliyeitwa **BAALI**.

Mfalme wa Israeli aliyeitwa Ahabu alimwoa Binti huyo wa kifalme na kumleta katika Taifa la Israeli na kuwa Malkia. Na hivyo kuingiza ibada za miungu migeni ndani ya Taifa la Mungu.

Yezebeli licha tu ya kulichafua Taifa la Israeli kwa kumshawishi sana Mumewe Ahabu, alikuwa pia ni mchawi (**2 Wafalme 9:22**). Aliwaua manabii wengi wa kweli wa Mungu, na aliikosesha Israeli kwa sehemu kubwa sana. Mahali pengine Inamtaja Yezebeli kuwa ni Nabii wa Uongo. (**Ufunuo 2:20**)

Yezebeli pia ndio mwanamke pekee kwenye Biblia nzima aliyekuwa anapaka **WANJA** usoni na kupamba uso. Desturi za wanawake makahaba. (**2 Wafalme 9:30**). Mwanamke huyu ndiye Mwanamke pekee aliyeshindana na maagizo ya Mungu kuliko wanawake wote kwenye Biblia, ndiye aliyemsumbua sana Eliya na hata kufikia hatua **Nabii Eliya** kumkimbia, kuogopa madhara atakayoyapata kutoka

kwake.

Yezebeli alikuwa na mtoto wa kike, aliyeitwa **ATHALIA** ambaye naye alirithi tabia zote za mama yake ambaye naye pia alikuwa anaabudu Baali, Athalia alikuwa muuaji na aliutwaa umalkia kwa nguvu ndani ya kabila la **YUDA**.

Yezebeli hakudumu muda mrefu kwani alikufa sawasawa na unabii uliotolewa juu yake, kwamba atakufa na mbwa watalamba damu yake. Siku ya kufa Yezebeli aliangukwa kutoka juu ya ghorofa refu na kuchuruza damu ukutani mwote, na alipofika chini farasi alimkanyaga kanyaga..na Mbwa walikumla na kubakisha viganja tu vya mikono na kifuvu (**2 Wafalme 9:35**)

jiunge na channel yetu Kwa kubofya hapa >> [WHATSAPP](#)

NABII ELIYA NI NANI?

*HATARI YA KUHUBIRI INJILI TOFAUTI NA ILIYOANDIKWA
KWENYE BIBLIA.*

USITAFUTE FAIDA YAKO MWENYEWE BALI YA WENGINE.

Rudi Nyumbani

Share on:
WhatsApp

[Print this post](#)